



UTAMADUNI WA VIJANA DUNIANI

Taarifa Ya Tanzania



Yaliyomo

3 UTANGULIZI

5 MITAZAMO & TABIA ZA KIDINI

16 USHAWISHI & SAUTI ZINAZOELEKEZA

23 UZOEFU & MING'ANG'ANO BINAFSI

30 MUUNGANIKO & MGUSO WA DIJITALI

39 UTAMBULISHO NA MAHUSIANO

45 KUZITAZAMA SIKU ZA MBELENI

48 KUHUSU ONEHOPE

48 KUHUSU UTAFITI

UTANGULIZI

Kila kizazi kipya ni cha kipekee kwa namna yake, na utafiti unaweza kutusaidia kuelewa ulimwengu unavyoonekana kupitia macho tofauti. Kizazi cha sasa cha watoto na vijana wakati mwingine kinaitwa Kizazi Z. Tanzania nzima, kuna zaidi ya vijana milioni 10 wa kizazi Z wenye umri kati ya miaka 13 -19 wakiwa 16% ya idadi ya watu.¹

Utafiti huu unaweka wazi tabia, ming'ang'ano, imani na ushawishi wa vijana Tanzania kote. Pia unaonesha mawazo ya vijana kumhusu Mungu, Yesu, Biblia, na kanisa. Takwimu zilikusanywa sehemu za vijijini, miji midogo, na mijini nchini Tanzania Julai 2022.

Utafiti huu ulikuwa wa kutathmini utafiti mkubwa wa dunia uliotafiti vijana kwenye nchi zaidi ya 20, zikiwepo nchi za Kenya, Nigeria, na Afrika Kusini. Toleo lililorekebisha la utafiti huu umefanyika kwenye nchi nyingine 10 za Kiafrika.




Tunatumaini kuwa si kwamba tu utajifunza jambo jipya, bali pia moyo wako utasukumwa kuchukua hatua kwa niaba ya kizazi hiki ambacho kinahitaji sana tumaini la Injili kwenye maisha yao.

Kila takwimu ya utafiti huu inawakilisha kijana mmoja na matumaini yake, hofu, na changamoto za kila siku. Kila mmoja wa hao vijana ana jina, hadithi, na hatima ya milele. OneHope imejitolea kugusa hatima hizi kwa kumfikia kila kijana kwenye kila nchi kwa neno la Mungu.

¹ United Nations Population Division, Total Population Database, <https://population.un.org/wpp/DataQuery/> Accessed September 2022

KUHUSU VIJANA




VIJANA **436**
WALIFANYIWA UTAFTI



WAVULANA: 45%
WASICHANA: 55%

ENEO²



DINI

WENGINE **17%**¹

WASLAMU **19%**



WAKRISTO **64%**



KAYA




52%
WAZAZI
WAWILI



13%
MZAZI
MMOJA



16%
WANAFAMILIA
WENGINE



19%
MAZINGIRA
MENGINE YA
KUISHI

¹ Vijana hawa walijitambulisha kama Mashahidi wa Yehova au Mormon na kwa kusudi la utafiti huu waliwekwa kundi tofauti na Wakristo.



² Kwa kusudi la utafiti huu eneo la vijijini lilifanuliwa kuwa na idadi ya watu ndogo kuliko watu 2,500, miji midogo watu 2,500-50,000, na eneo la mijini idadi ya watu zaidi 50,000.

MITAZAMO & TABIA ZA KIDINI

TAARIFA YA TANZANIA

Tuliyogundua

64% ya vijana Tanzania walijitambulisha kuwa **Wakristo**.



Ni **27%** ya vijana walionesha imani na tabia za **Wakristo Waliomaanisha**.

90% ya vijana wanaamini kuwa wanawajibika **kuishikirisha imani yao kwa wengine**.



Karibia **nusu** walisema kuwa mara kwa mara huwa na **mazungumzo** na wengine wasio wa imani yao.



27% ya vijana wa Kiislamu walikuwa tayari kuhudhuria ibada ya **Kikristo kwenye kanisa kama mtu akimwalika**.



Vijana Wakristo walitoa taarifa kuwa kanisa limekuwa na mchango **chanya kwenye makuzi yao ya kiroho**.




Vijana walisema wanaweza **kubadilisha imani** zao za dini kulingana na **mafundisho ya viongozi wa dini**.

Mitazamo & Tabia Za Kidini

Utafiti huu ulikuwa na ukubwa wa kipekee katika kupima mchango wa imani na dini kwenye maisha ya vijana hapa Tanzania.

Wanaamini nini? Wanawekaje imani yao kwenye matendo? Tulichunguza mitazamo na tabia za kidini ya vijana hawa na mguso wake kwenye maeneo mengine ya maisha.

UTAMBULISHO WA KIDINI



Wengi wa vijana waliochunguzwa Tanzania (64%) walitambuliwa kuwa Wakristo. Hii inakaribia takwimu rasmi zilizokadiriwa na kuonesha uhalisia wa dini Tanzania.

Vijana wa Tanzania pia walisema kuwa dini ni ya muhimu kwao. Kinachotia moyo, 96% wanasema imani yao au safari ya kiroho ni sehemu ya utambulisho wao. Kwa kuongezea, 90% ya vijana walikubali kuwa wanawajibika kushirikisha imani yao kwa wengine.


¹ Vijana hawa waliitambulisha kama Mashahidi wa Yehova au Mormon na kwa kusudi la utafiti huu waliwekwa kundi tofauti na Wakristo.

Lakini inamaanisha nini kuwa Mkristo halisi? Tulitazama misingi ya imani na vigezo vikuu vya nidhamu ya kiroho ambavyo vingionesha kuwa kijana ni Mkristo Aliyemaanisha.

SIFA 6 ZA VIJANA WAKRISTO WALIOMAA-NISHA



Tulipowapima vijana kulingana na tafsiri ya imani ya kumaanisha, mara moja tuliona tofauti kubwa. Tanzania nzima, vijana wachache walionekana kuwa Wakristo Waliomaanisha. Kila kijana wa Kikristo ambaye hakukidhi kimoja au zaidi ya vigezo vya kumaanisha alihesabiwa kuwa “Mkristo Jina” katika utafiti huu.




27% TU
YA VIJANA
WALIKUWA
WAKRISTO
WALIOMAA-
NISHA

Ingawa hili linaonekana kutuvunja moyo, ni muhimu kutambua kuwa Afrika ilikuwa na vijana zaidi walio Wakristo Waliomaanisha kwa dini zote kwenye utafiti wetu wa dunia. Kwa dunia, ni 7% ya vijana waliofanyiwa utafiti ni Wakristo Waliomaanisha.¹

¹ OneHope. (Agosti 2020). *Utamaduni wa Vijana Duniani, Taarifa ya Dunia*.
www.globalyouthculture.net


Hili bado ni pengo linalosumbua, hata hivyo, linaonesha kuna kazi ya kufanya katika kulea Wakristo kwenye misingi ya imani na tabia za imani yao. Pengo kati ya Wakristo Waliomaanisha na wa Jina lilionekana kwenye kila eneo la nchi.

WAKRISTO KWA ENEO




Namna Vijana Wanavyoitendea Kazi Imani yao

Kujikita katika nidhamu za kiroho ndiyo namna ya kukua kiroho. Tulitiwa moyo kuona vijana wengi Tanzania wanatoa kipaumbele kwa kutendea kazi imani zao katika ratiba zao za kila wiki.



¹ Jumla inazidi 100% kwa sababu ya kukadiria desimali.


Kumaanisha katika imani kulionesha tofauti kubwa kwenye maisha ya vijana na jinsi walivyochagua kutumia muda wao. Wakristo waliomaanisha walikuwa na uwezekano zaidi wa wenyewe kusoma Biblia, kwenda kanisani, kuomba, na kushirikisha imani yao.



42% YA VIJANA WAKRISTO HUONGELEA MAMBO YA DINI AU YA KIROHO KWA WATU WASIO WA IMANI YAO WALAU MARA MOJA KWA WIKI

Vijana na Kanisa


Vijana wengi Wakristo Tanzania (84%) walisema wanahudhuria ibada za dini walau mara moja kwa wiki. Kwa ujumla, vijana walitoa mrejesho chanya kuhusu nafasi ya huduma ya vijana kwenye maisha yao, na wengi wao kwa sasa wanapata malezi ya kiroho kwenye makanisa yao. Wasichana wana uwezekano zaidi kuliko wavulana kusema kuwa wanazungumza na viongozi wao wa kanisa kuhusu mambo yanayowahusu au yanayowasumbua.



Vijana wengi ambao kwa sasa hawaendi kanisani walisema wako tayari kwenda ikiwa mtu atawaalika (65%). Zaidi ya robo (27%) ya vijana wa Kiislamu walieleza kuwa wapo tayari pia kwenda kanisani. Tuligundua kuwa vijana wanaoishi kwenye vijiji vya Tanzania ni wachache waliokuwa wanaenda kanisani kulinganisha na wenzao kwenye maeneo ya miji midogo na miji mikubwa.

WALIKUWA WAZI KWENDA KANISANI

Nitakuwa tayari kuhudhuria ibada kanisani kama mtu ataniaalika.





UTAYARI WA KWENDA KANISANI KWA ENEO



65% YA VIJANA WANGEKWENDA KANISANI WAKIALIKWA

Maoni ya Kiroho

Wengi wa vijana waliotafitwa Tanzania walikuwa na maoni ya kiroho kumhusu Mungu, Yesu, na Biblia. Kinachotia moyo, hata baadhi ya vijana wa Kiislamu walikubali kuwa Yesu ni mwana wa Mungu na Biblia ni neno la Mungu. Wengi wa Waislamu, hata hivyo, walisema hawajawahi kufikiri kumhusu Yesu au Biblia.



Licha ya maoni ya jumla kuendana na Maandiko, bado kuna mkanganyiko kuhusiana na ukweli halisi. Vijana wachache sana wa Tanzania walisema kuwa dini zinafundisha kweli zilizo sawa. Hili haliendani na madai ya dini nyingi ukiwepo Ukristo kuwa wanafundisha kweli halisi.

Dini zote zinafundisha kweli sawa



Kinachobadilisha mawazo yao

Tulitaka kugundua mambo ambayo yangebadilisha mawazo ya vijana kuhusu dini waliyonayo. Jibu maarufu lilikuwa mafundisho ya viongozi wa dini. Hili lilikuwa tofauti na mwenendo wa dunia lakini limeonesha utamaduni wa Tanzania uliojengwa kijamii.

Vijana wa Tanzania walionekana kutoegemea uzoefu au uchunguzi binafsi. Badala yake, vijana walionekana kuwa na mwegemeo wa kijamii zaidi, wakisema kuwa wangewasikiliza kwanza viongozi wa dini, kisha marafiki au wazazi.


NI JAMBO GANI LINaweza
KUBADILISHA MAWAZO
YAKO KUHUSU IMANI YAKO
YA KIDINI?



- 1 MAFUNDISHO YA VIONGOZI WA DINI **46%**
- 2 MAZUNGUMZO NA MARAFIKI **22%**
- 3 MAZUNGUMZO NA WAZAZI **11%**
- 4 UCHUNGUZI WANGU BINAFSI MTANDAONI AU KWENYE VITABU **11%**
- 5 UZOEFU WANGU BINAFSI KAMA KUJIBIWA MAOMBI **10%**

Mpangilio wa vipaumbele ulikuwa sawa bila kujali jinsia ya kijana, eneo au dini. Hata hivyo, umri ulionekana kuwa kigezo cha ni nani vijana wanamsikiliza. Kulikuwepo na kushuka kwa ushawishi wa wazazi kwa vijana wakubwa (miaka 16-19). Vijana hawa wanawageukia zaidi viongozi wa dini na marafiki katika kujenga mawazo yao.

USHAWISHI KWA UMRI



Hitimisho

Takwimu hizi zinatunesha vijana wapo wapi kwenye safari ya kiroho na ukuaji na zinasaidia kuelewa utambulisho wao wa kidini, tabia, na maoni yao. Pia zinatuelekeza kwenye hatua za utendaji tunaposhirikisha Injili kwa wasioamini na kuwalea Wakristo Vijana wakomae katika imani.

- **KUWALEA WAKRISTO KUWA NA KINA KATIKA IMANI.**

Vijana wa Tanzania wanasema imani ni kitu muhimu kwao, na wengi wao ni Wakristo. Hata hivyo, hili halimaanishi kuwa kanisa libweteke. Utafiti wetu ulionesha kuwa wengi wa hawa waamini wana imani jina na wanahitaji kuendelea kulelewa kiroho. Tunawezaje kuwasaidia vijana hawa kukuza nidhamu za imani katika maandiko na kiroho zitakazowaondoa kuwa Wakristo Jina hadi waliokomaa na kustawi?

- **HIMIZA KUPENDA BIBLIA.**

Kusoma maandiko ni kitu ambacho kinapaswa kuhimizwa kwa vijana. Vijana wengi wanaojiita Wakristo ni nadra kuwa walishawahi hata kusoma Biblia yao. Tunawezaje kuwasaidia kizazi hiki kujihusisha na maandiko kila mara, kuyaruhusu kusema na mahitaji yao halisi na changamoto wanazokutana nazo maishani?

- **WAALIKE VIJANA KUJIFUNZA KUHUSU YESU.**

Vijana wengi walisema mafundisho ya viongozi wa dini yanaweza kubadilisha mawazo yao juu ya baadhi ya imani za dini. Baadhi kwenye kizazi hiki wamechanganyikiwa juu ya nini cha kuamini na iwapo dini zote zinafaa. Ni kwa jinsi gani tunaweza kufungua milango ya makanisa yetu na kuhakikisha vijana wanajisikia kukaribishwa na kualikwa kujifunza kuhusu Yesu, ambaye ndiye Njia, Kweli, na Uzima?

- **SAFARI YA PAMOJA.**

Inatia moyo kuona kuwa makanisa mengi yana wachungaji wa vijana na watu wazima wanaowekeza kwenye makuzi ya kiroho kwa kizazi kijacho. Walezi wa kiroho ni muhimu sana, hasa kwenye ujana ambapo maswali, hofu, na ming'ang'ano mara nyingi huibuka. Tunawezaje kuhakikisha kuwa kila kijana ana mtu fulani anayesafiri nao na ambaye wanajihisi salama kumshirikisha mahangaiko na changamoto zao?

- **KUWAWEZESHA VIJANA KUSHIRIKISHA.**

Karibia vijana wote waliotafitiwa wanaamini wanawajibika kuishirikisha imani yao kwa wengine. Hata hivyo, ni wachache ambao kiuhalisia wanashirikisha imani yao ya dini kwa wengine wasio wa imani yao. Ni kwa namna gani tunaweza kuwawezesha vijana kushirikisha tumani walilionalo katika Kristo kwa kizazi chao?

USHAWISHI & SAUTI ZINAZOELEKEZA


TAARIFA YA TANZANIA

Tulichogundua

Vijana wanasema
wazazi wao ndio **sauti**
zenye **ushawishi**
maishani wao.



86% ya vijana
wanaripoti **kuwa**
mahusiano na
familia zao ni
mazuri, lakini ni
nusu tu wanaishi
na **wazazi wao**.



92%

ya vijana wanaamini ni
muhimu **kuchangia**
kwenye ustawi wa
jumuia zao, na mitazamo
yao hubadilika kulingana
na umri.



Vijana wa kijijini wana **uwezekano**
kidogo kuliko vijana wengine
kuwa na **uhusiano wa karibu na**
mwanafamilia au rafiki.




Vijana wa mijini wana
uwezekano mkubwa
kutafuta **mwongozo**
kutoka kwenye familia,
wakati vijana wa kijijini
wanaegemea zaidi **viongozi**
au maandiko ya dini.

Marafiki na Mahusiano ya Familia

Tulipowauliza vijana ni nani anayeshawishi hatima zao za maisha, wazazi walikuwa chaguo kuu kwa wengi. Waalimu na ndugu wa kuzaliwa pia walitambuliwa kama mifano ya kuigwa. Tulitaka kujua kidogo kuhusu mahusiano ya vijana na wanaendeleaje?

NI NANI ANAYESHAWISHI HATIMA YAKO YA MAISHA¹



Zaidi ya nusu ya vijana waliotafitiwa Tanzania wanaishi na wazazi wote wawili. Hata hivyo, wengi wa vijana (86%) bado wana mahusiano mazuri na familia zao. Kinachotia moyo, vijana zaidi (76%) wanasema kuwa mara kwa mara huongea na wazazi wao kuhusu mambo muhimu kwao. Vijana ambao wamekuwa na mahusiano hasi na familia walikuwa na uwezekano mdogo wa kuwa na mazungumzo haya.

KAYA

Ninaishi na:



¹ Tambua kuwa vijana wangeweza kuchagua zaidi ya jibu moja kwa swali hilo.

MAZUNGUMZO NA WAZAZI

Ninazungumza na wazazi/walezi wangu kuhusu mambo muhimu kwangu



76% 18% 6%



Ninaongea na wazazi wangu kuhusu mambo muhimu kwangu


MAHUSIANO MAZURI YA FAMILIA: **77%**
MAHUSIANO MABAYA YA FAMILIA: **68%**

Takwimu hizi zinatuaonesha kwa kiasi fulani vijana wa kijijini wametengwa kwenye mahusiano ya familia na marafiki. Vijana wanaoishi vijijini walikuwa na uwezekano zaidi kusema kuwa wana mahusiano mabaya ya kifamilia (19%) kulinganisha na vijana wa maeneo mengine. Walikuwa pia na uwezekano zaidi kusema kuwa hawana marafiki wa karibu wanaowafahamu vema (22%).

Kinachotia moyo, wengi wa vijana Tanzania (81%) walionesha kuwa wana mahusiano imara ya kirafiki maishani mwao. Hata hivyo wasichana walikuwa wachache kulinganisha na wavulana kusema wana marafiki wanaowafahamu vema.

URAFIKI

Nina marafiki wa karibu wanaonifahamu vema



Vijana Wanaamini Familia

Vijana walituambia kuwa wanaziendea familia zaidi kuliko vyanzo vingine kupata mwongozo wa mada muhimu kama vile mema au mabaya. Familia zinabakia kuwa chanzo kikuu cha mwongozo wa vijana wanapohangaika kuhusu maana ya maisha. Familia inafuatiwa kwa karibu na viongozi na maandiko ya dini kwenye mada hizi.

MAZUNGUMZO YA JEMA NA BAYA

Ni wapi ninapoenda mara kwa mara kupata taarifa au mwongozo kuhusu lililo jema na baya

- 1 WANA FAMILIA **41%**
- 2 VIONGOZI/MAANDIKO YA DINI **40%**
- 3 WAALIMU/ WASHAURI **11%**
- 4 MARAFIKI/ KUNDI RIKA **4%**
- 5 VYOMBO YA HABARI VISIVYO VYA MTANDAONI¹ **3%**
- 6 MITANDAO YA JAMII/MTANDAONI **2%**


MAZUNGUMZO KUHUSU MAANA YA MAISHA

Ni wapi ninapoenda mara kwa mara kupata taarifa au mwongozo kuhusu maana ya Maisha

- 1 FAMILIA **41%**
- 2 VIONGOZI/MAANDIKO YA DINI **35%**
- 3 WAALIMU/ WASHAURI **12%**
- 4 VYOMBO YA HABARI VISIVYO VYA MTANDAONI **6%**
- 5 MARAFIKI/KUNDI RIKA **4%**
- 6 MITANDAO YA JAMII/MTANDAONI **2%**

¹ Inahusisha vitabu, majarida, Televisheni, redio, au magazeti


Vijana wengi maeneo ya vijijini ni wachache waliokuwa wanaziendea familia kupata mwongozo, na zaidi waliegemea viongozi na maandiko ya dini. Mtiririko huu ulikuwa tofauti maeneo ya mijini.



Vijana na Jumua

Pia tulidadisi namna vijana wanavyotazama mahusiano yao na jamua zao. Vijana wa Afrika walionekana kujikita zaidi kwenye jumua, na Tanzania ilifuata mtiririko huu. Wengi wa vijana (92%) walisema ni muhimu kwao kuchangia ustawi wa jumua zao. Kujihisi kuwajibika kulionekana kuongezeka na umri wa kijana.

Ni muhimu kwangu kuchangia ustawi wa Jamua yangu:



92% YA VIJANA WALISEMA NI MUHIMU KUCHANGIA USTAWI WA JUMUIA ZAO

Hitimisho

Kadri vijana leo wanavyochambua mambo na maswali magumu ya maisha, sauti wanazosisikiliza zinachanganya. Vyanzo ambavyo vijana wanaviamini na kuvigeukia vinatoa ishara ya watakachokiamini. Na unachokiamini kinaathiri sana namna utakavyoenenda.

- **FAMILIA INA JUKUMU LA KUTEKELEZA.**

Kinachotia moyo, vijana wanaripoti kuwa wazazi ndio washawishi wakuu kwenye maisha yao na vijana wanawaamini wanafamilia kuwaongoza katika maswali muhimu maishani mwao. Wazazi wasichukulie poa fursa walionayo ya kuzungumza kwenye maisha ya watoto wao. Tunawezaje kuzijengea uwezo familia kubeba wajibu wa kuwalea watoto na vijana wao ndani ya nyumba zao?

- **JAMII IMARA NI MUHIMU.**

Inatia moyo kuona kuwa vijana wengi wanasema wana marafiki wa karibu kama nyongeza ya mahusiano chanya ya familia. Hata hivyo, hili halikuwa kweli kwa vijana wa maeneo yote. Baadhi ya vijana walikosa watu wanaowafahamu vema na wanaoweza kuwasaidia wakati wanapokabiliana na changamoto. Tunawezaje kuwatia moyo vijana kuunganika na kushirikisha mambo nyeti kwa watu wanaoaminika maishani mwao?

- **THIBITISHA MAANDIKO KUWA MWONGOZO.**

Tulifurahi kuona kuwa vijana wamepandisha daraja viongozi na maandiko kama washawishi muhimu baada ya familia. Ni muhimu kwa vijana kuwa na kweli ya Mungu wanapouchambua ulimwengu huu unaoendelea kuwachanganya. Tunawezaje kuendelea kuwasaidia vijana waumini kuyaweka Maandiko kama mwongozo wao na kuelewa namna ya kulitendea kazi Neno la Mungu kwenye maisha yao kwa njia ya vitendo na inayobadilisha maisha?

- **TENGENEZA NJIA ZA KUCHANGIA.**

Takwimu zilionesha kuwa mahusiano ya jumua ni muhimu kwa kizazi hiki na vijana wanataka kufanya mema kwa jumua zao. Lakini watahitajika kuwezesha ili waweze kuchangia. Ni kwa namna gani tunaweza kutengeneza fursa kwa vijana ili waweze kuongoza na kutumika ndani ya jamii zao?

UZOEFU BINAFSI NA MING'ANG'ANO

TAARIFA YA TANZANIA

Tulichogundua



Baadhi ya vijana Tanzania wanang'ang'ana na **sonona na upweke**.



Vijana wa mijini wako kwenye **hatari kubwa kujiua** kuliko vijana wanaoishi maeneo mengine.



Vijana wakubwa walikuwa na uwezekano zaidi kuliko vijana wadogo **kung'ang'ana na afya ya akili**.



Vijana wanaong'ang'ana na **mambo ya ujinsia** wako kwenye hatari **kubwa zaidi ya kujiua**.



Wasichana walikuwa na uwezekano mara mbili zaidi kuliko wavulana kukumbana na **mawazo ya kujiua au hata kujaribu**.



Afya ya Akili

Tuliwauliza vijana kutueleza kuhusu uzoefu wao binafsi na ming'ang'ano waliyokumbana nayo kwenye maisha yao ndani ya miezi mitatu. Baadhi ya vijana wanaripoti upweke, fadhaa kuu, au sonona. Ingawa vijana Tanzania wanang'ang'ana na afya ya akili kwa kiwango kidogo kuliko wenzao kwenye nchi zingine za Afrika, viwango hivi bado ni vikubwa.

MING'ANG'ANO YA AFYA YA AKILI


Ndani ya miezi mitatu nimepitia:



Tofauti zilijitokeza tulipotazama takwimu kwa umri. Vijana wakubwa Tanzania wanang'ang'ana na afya ya akili zaidi kuliko vijana wadogo.

VIJANA WAKUBWA WANA MING'ANG'ANO ZAIDI

Ndani ya miezi mitatu nimepitia:




Kujua


Tuliwauliza vijana iwapo binafsi, ndani ya miezi mitatu, wamekumbana na mawazo ya kujiua au kufanya jaribio la kujiua. Kinachohuzunisha ni kuwa, baadhi ya vijana walitueleza kuwa walikumbana na hali hii. Hatari ya kujiua ilihusiana kwa karibu na eneo, vijana wa mijini wakiwa na uwezekano mkubwa wa ming'ang'ano hii. Wasichana walikuwa na uwezekano mara mbili zaidi kuliko wavulana kuwa na mawazo ya kujiua au hata kufanya jaribio kwenye maisha yao.

Ndani ya miezi mitatu nimepitia:

MAWAZO YA KUJIUA




MAJARIBIO YA KUJIUA



HATARI YA KUJIUA KWA ENEO

Ndani ya miezi mitatu nimepitia:




MAWAZO YA KUJIUA



Hatari ya kujiua imeunganika kwa karibu na ming'ang'ano mingine inayowakumba vijana. Utafiti wetu unaonesha vijana wa Tanzania wanaopambana na mambo ya ujinsia wako hatarini zaidi kukumbwa na mawazo ya kujiua au kufanya jaribio. Kati ya vijana walioripoti kuvutiwa na mapenzi ya jinsia moja, 42% kati yao wamekumbwa na mawazo ya kujiua na 33% wamefanya jaribio. Kutazama picha za ngono na kushiriki ngono yameunganika kwa karibu na hatari ya kujiua, sawa sawa na kunyanyaswa au kuwa na fadhaa kuu.

MIUNGANIKO 5 YENYE HATARI YA KUJIUA



Sio lazima kuwa tukio moja au uzoefu ndio unasukuma vijana kujiua, lakini inaweza kuwa mtiririko wa hatua ndogondogo na mawazo yanayojenga juu ya mengine. Pasipo kurejea tukio fulani, takwimu hizi zinatuonesha kuwa vijana wako katika giza kubwa linalowasukuma kuelekea kwenye vitendo hatarishi.

Lazima tuguswe na vijana wanaoumia sana kiasi cha kutaka kujiua. Inapofikia suala la kujiua, hatuungalii namba kwenye ukurasa — bali maisha halisi ya watu. Idadi yoyote ni kubwa sana na asilimia yoyote kubwa sana.


Ming'ang'ano Mingine

Changamoto wanazokumbana nazo vijana sio mara zote zinaonekana kwa nje. Lakini zinaweza kuwa na udhihirisho wa nje. Vijana wachache wa Tanzania waliripoti kuwa hivi karibuni wamelewa na kutumia madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya yalionekana kuwa tatizo kwenye miji midogo, na wasichana wakiathirika zaidi ya wavulana. Wavulana, kwa upande mwingine, walikuwa mara mbili zaidi ya wasichana kutazama picha za ngono hivi karibuni.

Unyanyasaji ulikuwa changamoto nyingine dhahiri kwa kizazi hiki. Karibia kijana 1 kati ya 5 waliripoti kuwa walipitia hili karibuni, unyanyasaji ukiwa jambo la kawaida kwa wasichana kuliko wavulana. Takwimu hizi zilitukumbusha kuwa miaka ya ujana inaweza kuwa na ming'ang'ano binafsi na ya umma ambayo inaweza kuathiri ustawi wa kizazi hiki.


MATUMIZI YA POMBE NA DAWA ZA KULEVYA

Ndani ya miezi mitatu iliopita nimepitia:



MING'ANG'ANO KWA JINSIA

Ndani ya miezi mitatu iliopita nimepitia:



Hitimisho

- **AFYA YA AKILI NI MUHIMU.**

Utafiti huu uwe kengele ya kutuamsha kuhusu ming'ang'ano wanayokumbana nayo vijana na jinsi ambavyo vyote vinafanya kazi kuwaangusha. Tunahitaji kuwasaidia vijana wakubwa wanaokumbana na madhara hasi kwa kiwango kikubwa. Tunawezaje kuwasaidia kuhisi wanaonekana, kusaidika, na kutiwa moyo kwa tumaini la Injili wanaloshikilia kwenye maisha yao?

- **HATARI YA KUJIUA NI KUBWA.**

Baadhi ya vijana wanajihisi kukata tama na hata kufikiria kuhitimisha maisha yao. Vijana wanaoishi kwenye miji mikubwa ndio wanaokumbwa zaidi na mawazo ya kujiua na hata kujaribu kujiua. Pia inaonekana kuna shinikizo linalozunguka jinsia ambalo linawaathiri zaidi wasichana kuliko wavulana. Ni kwa namna gani tunaweza kuwa macho kuhusu changamoto hizi na kuhakikisha kuwa vijana wanafahamu tunajali kila eneo la maisha yao?

- **MING'ANG'ANO IMEUNGANIKA.**

Vijana inaonekana wanang'ang'ana kwenye maeneo mengi maishani mwao. Mambo ya ujinsia yameunganika na hatari kuu ya kujiua. Tunapaswa kufikiri kwa umakini mazingira tunayowatengenezea kizazi hiki ambayo yanakuza changamoto hizi. Ni kwa namna gani tunaweza kuwatia moyo kutafuta msaada, kuliko kuficha changamoto zao, na kuhakikisha wanahisi kusaidiwa kuliko kuaibishwa kwa mawazo na vitendo vyao?



MUUNGANIKO WA KIDIJITALI NA MGUSO WAKE

TAARIFA YA TANZANIA

Tulichogundua



Nusu ya watumiaji wa simu janja wanasema wanakuwepo mtandaoni walau mara **moja kwa wiki**.

Muunganiko wa kidijitali na muda wa kuwa mtandaoni unaongezeka kwa vijana **wanaoishi mijini**.




42% ya vijana **wanamiliki simu**, nyingi zikiwa simu janja.



Baadhi ya vijana wanatambua kuwa kuwepo mtandaoni kunawapokonya **muda muhimu wa shughuli za nje ya mtandao**.



Vijana wamegawanyika juu ya athari za **mitandao ya jamii** kwenye maisha yao, wanaripoti athari zote **chanya na hasi**.




Vijana wengi (**64%**) wanasema wapo mtandaoni kwa sababu **wanataka kuwepo**, sio kwa sababu wanalazimika.





Vijana na Teknolojia

Intaneti ni kitu ambacho kinaonekana kujenga kizazi hiki. Vijana wanaweza kupata taarifa, maoni, na ushawishi kwenye ncha ya vidole vyao. Lakini kwa namna gani hili linaathiri vijana Tanzania?

Tulitaka kufahamu ni vijana wangapi wana simu, muda kiasi gani wanautumia mtandaoni, na namna wanavyotumia mitandao ya jamii. Asilimia Arobaini na mbili ya vijana wa Tanzania waliofanyiwa utafiti walisema wana simu. Kati yao, zaidi ya nusu (56%) walisema wana simu janja.




NINAMILIKI SIMU




Kwa vijana waliunganishwa na intaneti, wengi hutumia vifaa vyao binafsi kama simu janja kuingia mtandaoni. Lakini vijana wanalazimika kutumia kifaa au kutumia vifaa vya umma. Wengi wanasema wanaingia mtandaoni wakiwa nyumbani.

Baadhi wanasema fursa tu walionayo ni kupitia simu ya mkononi. Vijana wachache wanalazimika kutoka nje ya nyumbani kwenye vibanda vya intaneti, kanisani, au shuleni ili kupata intaneti.

Jumla inazidi 100% kwa sababu ya kukadiria desimali?



Ni wapi unapata intaneti?²




¹ Jumla inazidi 100% kwa sababu ya kukadiria desimali.


² Tambua kuwa vijana wangeweza kuchagua zaidi ya jibu moja kwa swali hilo.

Upatikanaji wa intaneti haujaenea kwa vijana Tanzania. Vijana wachache walisema wanakuwa mtandaoni kila siku. Wengi (65%) walisema hawapo mtandaoni. Hili lilibadilika kulingana na eneo na jinsia. Wasichana walikuwa na uwezekano mdogo zaidi kumiliki simu au kupata intaneti kuliko wavulana. Vijana wanaoishi maeneo ya vijijini walikuwa na uwezekano mdogo kuunganishwa kwenye intaneti kuliko vijana wa mjini. Kwa ujumla watumiaji wa Simu Janja walikuwa na uwezekano zaidi kuwa mtandaoni.

NI MARA NGAPI UNAPATA INTANETI?



UPATIKANAJI WA INTANETI KWA ENEO





¹ Jumla inazidi 100% kwa sababu ya kukadiria desimali.

Vijana na Interneti

Ni kiasi gani cha muda vijana wanachotumia mtandaoni, na wanafanya nini huko? Vijana waliofanyiwa utafiti Tanzania waliripoti kutumia saa moja na nusu kwenye kila kipengele cha shughuli za mtandaoni tulichohoji. Vijana wa mjini, hata hivyo, walitumia muda mwingi zaidi kuliko wenzao kwenye mitandao ya jamii na kucheza michezo.

Katika siku ya kawaida, kwa wastani ni masaa mangapi unayatumia mtandaoni?




Tulikuwa pia wadadisi kuhusu uzoefu wa kuwa mtandaoni na kama ni kitu ambacho vijana wanahisi kina mchango chanya kwenye maisha yao.

Vijana wengi (64%) wanasema wanaenda mtandaoni kwa sababu wanajisikia. Hata hivyo, wasichana walikuwa na uwezekano wa kujisikia kulazimika kuwa mtandaoni na kuripoti kuwa mitandao ya jamii ina mchango hasi kwao.

Kwa ujumla 23% ya vijana wanatambua kuwa kwao mtandaoni kunawapokonya muda mzuri wa shughuli za nje ya mtandao kama kufanya mazoezi, kuwaona marafiki, kusoma, au kulala.


Hili linadhihirisha kuwa kizazi hiki kinafahamu athari kinazopata kutokana na muunganiko huu wa kidijitali. Vijana wakubwa walikuwa na uwezekano zaidi kusema kuwa muda wao mtandaoni una athari zaidi kulinganisha na vijana wadogo. (28% kwa 18%).

NIPO MTANDAONI WA SABABU...¹




NINATAKA KUWEPO
NAHISI KULAZIMIKA KUWEPO
VYOTE

MUDA NINAOTUMIA MTANDAONI UNANIPOKONYA MUDA MZURI WA SHUGHULI ZA NJE YA MTANDAO




NIPO MTANDAONI
KWA SABABU
NINATAKA
KUWEPO



Wavulana Wasichana



MITANDAO YA
JAMII INANIFANYA
NIJISIKIE HUZUNI,
FADHAA, AU SONONA:



Wavulana Wasichana

¹ Jumla inazidi 100% kwa sababu ya kukadiria desimali.



Vijana na Mitandao ya Jamii

Linapokuja suala la mitandao ya jamii, vijana waligawanyika sana kuhusiana na madhara yake kwenye maisha yao. Zaidi ya nusu (58%) walisema inawasaidia kupata ridhiko la maisha yao, lakini idadi ya kutosha (42%) pia ilisema inawafanya wajisikie huzuni, fadhaa, au sonona. Wasichana walikuwa na uwezekano zaidi ya wavulana kutambua hayo madhara hasi. Vijana wengi walisema wanatumia mitandao ya jamii kuwasaidia kupata taarifa.




Mitandao ya jamii inanisaaidia kupata ridhiko la maisha.



Mitandao ya jamii inanifanya nijisikie huzuni, fadhaa, au sonona.



NINATUMIA MITANDAO YA JAMII¹ KIMSINGI



1 Tambua kuwa vijana wangeweza kuchagua zaidi ya jibu moja kwa swali hili.

Hitimisho

Kuunganika mara kwa mara kwenye majukwaa ya kidijitali unakuwa mtindo wa maisha kwa vijana wa leo. Tanzania haiko nyuma katika hili. Idadi ya vijana wanaomiliki simu na kuunganishwa na mtandao wa intaneti nchi nzima inaongezeka. Tutawasaidiaje kuchambua uhalisia huu mpya na kuwafikishia Injili ipasavyo kwenye majukwaa haya ya kidijitali?

- **KUZIFAIDI FURSA ZA KIDIJITALI.**

Teknolojia inaweza kuwa zana yenye nguvu kukifikia kizazi hiki. Vijana wengi, haswa katika miji yetu, wanaingia mtandaoni na kuzifaidi programu, tovuti, na majukwaa ya mitandao ya kijamii inayopatikana. Ni kwa namna gani tutahakikisha kuwa wanapata maudhui ya Injili na jumua zenye uzima wanazoweza kuwa sehemu yake?

- **CHAMBUA MASUMBUFU.**

Wakati kizazi hiki kinaonekana kukumbatia dijitali, baadhi ya vijana wanatambua usumbufu ambao vifaa hivi unaleta kwenye maisha yao. Wasichana wanahisi matokeo haya hasi zaidi kuliko wavulana, na vijana wakubwa wanahisi huo mgawanyiko kati ya uhalisia wao wa mtandaoni na nje ya mtandao. Tunawezaje kutumia mabadiliko ambayo dijitali inaleta na kuwasaidia vijana kuchambua ushiriki wao kwa njia yenye afya?

- **JIZATITI KWA MAISHA YA MBELEN.**

Muunganiko wa kidijitali ndio maisha ya mbeleni ambayo tunayaendea, na vijana wanaongoza katika hili. Hatuwezi kuzuia hili, lakini tunaweza kusafiri nao kuliko kuwapoteza kwenye ulimwengu wa dijitali ambao sisi sio sehemu yake na hautuelewi. Kama familia, viongozi wa kanisa, na watenda kazi wa huduma tunahitaji kutambua jinsi ulimwengu unavyobadilika na namna ambayo tunapaswa kubadilika nao. Tunawezaje kukumbatia dijitali sambamba na kizazi hiki na kuleta hekima na uvumbuzi kwenye anga hili?

UTAMBULISHO NA MAHUSIANO

TAARIFA YA TANZANIA

Tutichogundua

64% ya vijana wanaamini jinsia ya **mtu ni ile aliyozaliwa nayo...**




...lakini **wengi wamechanganyiki** wa kuhusu mada hii.



Ni vijana **wachache** walioripoti wao binafsi kuvurugwa na **utambulisho wa kijinsia.**



Waalimu ndio wenye **ushawishi zaidi** kwa vijana juu ya mada za **utambulisho wa jinsia** na ujinsia, ilihali ushawishi wa **viongozi na maandiko ya kidini umeshuka.**



Vijana wengi (**64%**) walisema ndoa yapaswa kuwa uhusiano **wa muda mrefu**, lakini wengi baadhi wanasema **hawana uhakika.**

Wavulana

wana uwezekano zaidi kuliko wasichana kuona ni sawa **kujamiiana kabla ya ndoa.**



Mitazamo Juu ya Utambulisho wa Kijinsia


Mazungumzo juu ya utambulisho wa jinsia na ujinsia yanakuwa jambo la kawaida katika kizazi hiki. Tulitaka kufahamu mitazamo ya vijana ya Tanzania.

Wengi walisema jinsia ya mtu ni ile aliyozaliwa nayo. Hata hivyo, idadi ya kutosha ya vijana walisema hili swali limewachanganya, kitu kinachoashiria kuwa haya sio mazungumzo ya kawaida kwao. Vijana wengi sana walisema hawajakumbwa na aina yoyote ya mvurugo wa ujinsia maishani mwao.


MTAZAMO WA JINSIA

Jinsia imejengwa kwenye:

JINSIA MTU ALIYOZALIWA NAYO NAMNA JAMII INAVYOMUONA MTU
KUJISIKIA AU KUTAMANI SWALI HILI LIMENICHANGANYA



Je, umekumbana na mvurugo wa utambulisho wa jinsia ndani ya miezi mitatu iliyopita:



Ushawishi kwenye Maongezi

Vijana waliulizwa kutushirikisha wanakoenda kupata mwongozo kuhusu mada kubwa za jinsia, ujinsia, na mambo ya kujamiiana.

Vijana walisema kuwa mara nyingi wanawaendea walimu au washauri kupata mwongozo kwenye mada hizi, ikifuatiwa na wanafamilia. Takwimu zilionyesha kuwa vijana wanaegemea mahusiano ya mtu na mtu kwa mwongozo kuliko kuiendea mitandao. Hata hivyo, iligundulika kushuka kwa kiwango cha ushawishi wa viongozi wa dini kulinganisha na mamlaka waliokuwa nayo kwenye mada zingine (tazama sehemu ya Ushawishi na Sauti Zinazoelekeza).

USHAWISHI JUU YA MITAZAMO YA JINSIA



Wapi ninapoenda mara nyingi kupata taarifa au mwongozo kuhusu jinsia, ujinsia na mambo ya kujamiiana.

- 1 WAALIMU/WASHAURI **31%**
- 2 FAMILIA **27%**
- 3 MARAFIKI/KUNDI RIKA **14%**
- 4 VIONGOZI/MAANDIKO YA DINI **14%**
- 5 VYOMBO YA HABARI VISIVYO VYA MTANDAONI **9%**
- 6 MITANDAO YA JAMII/MTANDAONI **7%**

USHAWISHI JUU YA MITAZAMO YA JINSIA



WAALIMU/WASHAURI

41%

VIJIJINI

27%

MIJI MIDOGO

23%

MIJI MIKUBWA



FAMILIA

15%

VIJIJINI

31%

MIJI MIDOGO

35%


MIJI MIKUBWA

Ushawishi ulionekana kubadilika kulingana na eneo.

Vijana wa maeneo ya kijijini walionekana kuegemea zaidi waalimu wao, wakati vijana wa mijini walionekana kuegemea kwenye ushauri wa familia.

Mitazamo ya Ndoa

Je, ndoa inapaswa kuwa Uhusiano wa Kudumu



Tulichunguza imani za vijana kuhusu ndoa.

Wengi wa vijana Tanzania (64%) walisema ndoa inapaswa iwe mahusiano ya kuduma. Hata hivyo, idadi kubwa haikuwa na uhakika.

Ndoa inapaswa kuwa ya Uhusiano wa Kudumu

13-15



16-17



18-19




Mitazamo iliendana na umri, vijana wakubwa walikuwa na uhakika zaidi kuwa ndoa inapaswa kuwa ya maisha yote.


Vijana Tanzania walisema pia kuwa sio sawa kujamiiana kabla ya ndoa.

Je, unaamini ni sawa kujamiiana kabla ya ndoa?

NDIYO HAPANA
LABDA



NDIYO AU LABDA



Hata hivyo, kulikuwa na tofauti ya maoni kulingana na jinsia na eneo. Wavulana walikuwa na uwezekano zaidi kuliko wasichana kusema kuwa inaweza kukubalika, pamoja na vijana wa meneo ya mijini.

NDIYO AU LABDA



VIJIJINI



MIJI MIDOGO



MIJI MIKUBWA

Hitimisho

Maoni ya mtu hayadumu milele, lakini kwa sasa tunafahamu vema kile ambacho vijana hapa Tanzania wanaamini juu ya mada muhimu kama utambulisho wa jinsia, ujinsia, na ndoa. Kwa nyongeza, tunafahamu wanakogeukia kupata mwongozo na ushauri wa mambo haya.

- **IMARISHA MITAZAMO YA KIMAANDIKO.**

Inatia moyo kuona kuwa vijana wa Tanzania wana mitazamo ya kimaandiko juu ya mada kama utambulisho wa jinsia, ujinsia, na ndoa. Lakini mada hizi zinapaswa kuendelea kuzipalilia kadri vijana wanavyokua na kuanza kusikia maoni na sauti zingine. Tunawezaje kuwasaidia vijana kuelewa mpango wa Mungu alionao kwa ujinsia na mahusiano yao na hivyo kuuishi muundo huu ili waweze kustawi?

- **JINDAE KWA MAZUNGUMZO YANAYOCHANGANYA.**

Sauti za utamaduni zinazungumza na vijana kwa nguvu kupitia muziki, vyombo vya habari, na majukwaa ya kidijitali. Lakini utamaduni utaendelea kuwa mbali na maadili ya Ki-Mungu. Tunapaswa kujiandaa wenyewe na kizazi hiki kwa mazungumzo ya wazi juu ya mada za utambulisho wa jinsia, mvuto wa mpenzi ya jinsia moja, na ngono nje ya ndoa. Tunapaswa kuwa tayari sio tu kuisema kweli ya Mungu lakini pia kuwa wasikilizaji wazuri wa vijana wanaoweza kuhisi kuchanganyikiwa au kuwa na hofu kwenye mada hizi.

- **KUZENI USHAWISHI WA KANISA.**

Wachungaji na viongozi wa kanisa wanatambuliwa kuwa na nguvu kwenye mada juu ya jema na baya na maana ya maisha, lakini ushawishi wao umepungua kwenye maeneo mengine ya mazungumzo ya kiutamaduni. Vijana wanaishi kwenye ulimwengu unaozidi kukua na kuchanganya kila siku, lakini wanapaswa kujua kuwa Neno la Mungu linasema na kila eneo la maisha yetu. Tunawezaje kuwasiliana na kizazi hiki na kulifanya kanisa liwe sauti inayoaminika na mahali salama kwa kila kijana kuchambua maswali juu ya jinsia na ujinsia?

- **MALEZI YA KIROHO KWA FAMILIA.**

Vijana wanawatazamia watu wazima kwenye maisha yao kuwapa mwongozo kwenye mada hizi, na wanafamilia ndiyo mwongozo muhimu zaidi. Vijana mara nyingi hufuata wazazi wao kwenye imani na mitazamo. Tunawezaje kulea kiroho familia nzima kuwa na mtazamo wa Ki-Mungu juu ya jinsia na ujinsia?



KUTAZAMA MBELENI

TAARIFA YA TANZANIA

Takribani vijana wote Tanzania wanaona elimu kuwa ufunguo wa mafanikio yao ya mbeleni. Asilimia tisini na nane wanasema elimu ndio kitu cha msingi kitakachowahakikishia maisha bora ya mbeleni. Vijana wengi hawatarajii jambo lolote kuwakwamisha kwenda chuo kikuu. Kati ya wale walioona vikwazo, gharama ilitajwa mara nyingi. Asilimia 33 ya vijana walisema kuwa inaweza kuwakwamisha kwenda chuo kikuu.

Vijana wadogo walikuwa na ujasiri zaidi kuwa wangeweza kwenda, kulinganisha na vijana wakubwa ambao walisema inagharimu mno. Kwa ujumla, ilitia moyo kuona kuwa vijana hawakutiwa shaka na vikwazo kama muda, matakwa ya chuo, au kumudu kuingia chuo kikuu.

NI NINI KITAKACHOKUZUIA KWENDA CHUO KIKUU?¹



1 Tambua kuwa vijana wangeweza kuchagua zaidi ya jibu moja kwa swali hili.



Kazi za Mbeleni

Ingawa inawezekana wasielewe kilichopo mbele, vijana wanajua wanachotaka kwenye kazi zao za mbeleni. Vipaumbele vyao ni kuwa watakuwa wanawasaidia wengine, ikifuatiwa na shauku ya kuwafanya wazazi wao wafurahi. Ni kiasi gani inalipa na iwapo au inaheshimika au wanaifurahia havikuwasumbua. Vipaumbele hivi vilifanana pasipo kujali umri, jinsia, au eneo alilopo kijana.

95% YA VIJANA TANZANIA WANA MALENGO YA KUWA WAJASIRIAMALI

Vijana Afrika ni baadhi ya wenye hamasa kuu kwenye kizazi cha dunia kwa kuwa na shauku ya kuwa wajasiriamali. Hili lilikuwa hivyo hata Tanzania. Karibia vijana wote waliotafitiwa (95%) walisema wangetamani kuanza biashara au kumiliki kampuni zao hapa mbeleni.

VIPAUMBELE VIKUU VYA KAZI



Kuhusu OneHope

Kwa kushirikiana na makanisa ya mahali, huduma na serikali duniani kote, OneHope imefikia zaidi ya watoto na vijana bilioni 1.7 kwa Neno la Mungu. Kulingana na utafiti wa nchi ambao OneHope inaufanya, programu za Maandiko zimeundwa kwa kuzingatia umri na utamaduni wa nchi husika. Tangu 1987, OneHope imesaidia watoto kuifahamu hadithi ya Mungu, kushirikisha watoto na vijana wa kila nchi ujumbe wa tumani linalobadilisha. onehope.net

Kuhusu Utafiti

Mradi huu uliendeleza utafiti wa dunia uliochunguza vijana wa umri wa 13-19 kwenye nchi zaidi ya 20. Utafiti huu wa dunia ulifanyika Februari-Machi mwaka 2020. Utafiti wa mradi huu ulifanyika Julai 2022.

Takwimu zinawakilisha maeneo mbali mbali na mikoa yote Tanzania na maswali yaliulizwa kuendana na mazingira ya Kitaifa. Vijana walitaftiwa mmoja mmoja shuleni na waliandika majibu yao kwenye karatasi. Kwa sababu ya tofauti hii sio kila kijana alipaswa kujibu kila swali. Hata hivyo, ukubwa wa sampuli ulitosha kwa kila swali lilipo kwenye taarifa hii.

MKRISTO

Vijana waliojitambulisha kuwa Wakristo, lakini sio Mashahidi wa Yehova au Mormon.

WAKRISTO WALIOMAAANISHA

Vijana waliojitambulisha kuwa Wakristo, lakini sio Mashahidi wa Yehova au Mormon, na ambao walikidhi vigezo vifuatavyo:

- Wanaamini kuwa Mungu yupo na wanaweza kuwa na mahusiano binafsi na Yeye.
- Wanaamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu.
- Wanaamini kuwa msamaha wa dhambi unawezekana tu kupitia imani katika Yesu Kristo.
- Wanaamini kuwa Biblia ni Neno la Mungu.
- Wanasoma Maandiko wenyewe walau mara moja kwa wiki.
- Wanaomba walau mara moja kwa wiki.

Tambua kuwa vijana Wakristo Waliomaanisha wanaweza kuwa Wakatoliki.

WAKRISTO JINA

Vijana waliojitambulisha kuwa Wakristo, lakini sio Mashahidi wa Yehova au Mormon na ambao hawakukidhi vigezo msingi vya imani au tabia zilizoainishwa kwa Wakristo Waliomaanisha.

Hakimiliki © 2022 OneHope, Inc

Nukuu zinazopendekezwa:
OneHope. (Oktoba 2022). Utafiti wa Utamaduni wa Vijana Duniani, Ripoti ya Tanzania
www.globalyouthculture.net



UTAMADUNI WA VIJANA DUNIANI